



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEUZI WA WAGOMBEA

WA KITI CHA RAIS, MAKAMU WA RAIS, WABUNGE NA

MADIWANI

Dodoma, Jumatatu 24 Agosti, 2020

Kesho tarehe 25 Agosti, 2020, Tume ya Taifa ya Uchaguzi itafanya uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wabunge na madiwani nchi nzima.

Uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais utafanyika katika ofisi za Tume zilizopo eneo la Njedengwa Mkoani Dodoma. Aidha, uteuzi wa wagombea ubunge utafanyika katika ofisi za Wasimamizi wa Uchaguzi wa Majimbo husika na kwa wagombea udiwani uteuzi utafanyika katika ofisi za Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata.

Hadi hivi leo, wagombea wa vyama vya siasa 17 vyenye usajili wa kudumu wamechukua fomu za uteuzi wa kiti cha Rais na makamu wa Rais. Kwa upande wa ubunge na udiwani, Tume inaendelea

kukusanya taarifa za waliochukua fomu baada ya kupendekezwa na vyama vya siasa.

Kesho tarehe 25 Agosti, 2020 ndiyo siku ya uteuzi. Baada ya zoezi la uteuzi, fomu zitabandikwa katika mbao za matangazo za ofisi iliyohusika na uteuzi. Kwa mujibu wa kanuni ya 29 ya kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 27 ya kanuni za Uchaguzi wa Madiwani za mwaka 2020, fomu hizo zitawekwa eneo la wazi hadi saa 10 kamili jioni tarehe 26 Agosti, 2020, ambapo wagombea watapata nafasi ya kuweka pingamizi. Wengine wanaoruhusiwa kuweka pingamizi ni Mkurugenzi wa Uchaguzi, Wasimamizi wa Uchaguzi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Msajili wa Vyama vya Siasa.

Aidha, Tume inaelekeza na inawasisitiza Wasimamizi wa Uchaguzi wa majimbo na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata kuwepo kwenye Ofisi zao kesho wakati wote kuanzia saa 1 asubuhi hadi saa 10 jioni. Kitendo cha kutokuwepo ofisini katika muda huo kitapelekea Tume kuchukua hatua kali dhidi ya watendaji wa majimbo na kata husika.

Kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi kampeni za uchaguzi zinatarajiwa kuanza tarehe 26 Agosti, 2020 hadi saa 12 jioni tarehe 27

Oktoba 2020, ikiwa ni siku moja kabla ya Siku ya uchaguzi yaani tarehe 28 Oktoba 2020. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Kampeni zitahitimishwa tarehe 26 Oktoba, 2020 ili kupisha upigaji kura wa awali.

Tume inawakumbusha wahusika wa Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kutii, kuheshimu na kuzingatia Maadili, Sheria, Kanuni na taratibu zilizowekwa, yakiwemo makatazo mbalimbali yaliyomo katika Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020.

Tume inarudia kuvikumbusha vyama vya siasa kuzingatia maelekezo yaliyomo katika Maadili ya Uchaguzi hasa katika eneo la kuzitumia kamati za maadili kutatua migogoro na malalamiko yatakayojitokeza.

Tume kwa upande wake itaendelea kuzingatia Katiba, Sheria, kanuni za uchaguzi na maelekezo yaliyomo katika Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020.

(signed)

Jaji wa Rufaa (Mst.) Semistocles Kaijage

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI